

i. إِدْغَامُ الشَّوِيِّ Idghaam Ash-Shafawy

Hukmu hii hutokea pale zinapokutana miym saakinah (م) na miym yenye *i'raab*, kwa sharti kwamba miym ya kwanza ndio iwe na sukuwn. Hivyo, itapokuja baada ya miym saakinah (م) miym yenye *i'raab*, basi miym ya kwanza ambayo ni saakin huingizwa katika miym ya pili yenye *i'raab*, na kupelekea kuwa miym moja iliyo na shaddah na yenye ghunnah. Hii pia huitwa إِدْغَامُ الْمُتَمَاتِلَيْنِ (Idghaamul-mutamaathilayni).

Mifano ya idghaamu shafawiy	
Inavyotamkwa	Mfano
kuntummuuniyn	كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ
wa aamanahummin khawf	وَأَمَانَهُمْ مِنْ خَوْفٍ
wa hummuhtaduwn	وَهُمْ مُهْتَدُونَ
ya'idukummaghfirah	يَعِدُّكُمْ مَغْفِرَةً
Rabbihimmin kulli amr	رَبِّهِمْ مِنْ كُلِّ أَمْرٍ
ilaa Rabbihimmarji'uhum	إِلَى رَبِّهِمْ مَرْجِعُهُمْ